

Je, nini kipya?
Sauti za Wananchi
...njia poa ya kusikika!

Kijitabu hiki kimechapishwa na Twaweza Afrika Mashiriki, 2019

Mchoraji: Marco Tibasima

22 School Lane, Westlands
Kitalu B, Ghorofa ya 2
SLP 13784-00800
Nairobi Kenya.
Namba za simu: +254 786 563 722, +254 715 563 720
Barua pepe: info@twaweza.org
Tovuti: www.twaweza.org
Twitter: @Twaweza_Ke
Facebook: Twaweza Kenya
Instagram: Twaweza East Africa

*Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba umebainisha sehemu kamili uliyoinakili na kutambua Twaweza.*

Twaweza
ni sisi

**Mpendwa Msomaji,**

Kila mmoja wetu ana jambo la kusimulia: kuhusu tunapoishi, mambo mapya kwenye maisha yetu na nini tunachotaka kubadilisha. Tuna sauti lakini mara nyingi sauti hizi hazisikiki kwa watu wengine mbali na marafiki na familia. Lakini wengi wetu hatujui kwamba ukweli wa hali halisi ni kivutio kwa watu wengi; kwa wananchi wa kawaida na pia kwa viongozi wanaotuwakilisha.

Pindi Sauti za Wananchi zinaposikika, ukweli wa maisha yao unaweza kusaidia kulijenga taifa. Kijitabu hiki kinahusu jitihada mpya inayoitwa “Sauti za Wananchi”, iliyoandaliwa na shirika huru liitwalo Twaweza. Mpango huu ulitekelezwa katika ngazi ya kitaifa kuanzia mwaka 2015, sasa unatekelezwa katika ngazi ya kauti, ikianza na kauti hii ya Makueni.

Kijiji chako au mtaa ni moja ya maeneo 70 yaliyochaguliwa kinasibu katika mpango huu. Katika kila  eneo, washiriki kumi na wawili wamechaguliwa kinasibu. Mara moja au mbili kila mwezi, Twaweza itawapigia simu washiriki na kuwauliza maswali machache.

Lengo ni kujifunza kuhusu hali ya maisha na maoni ya wananchi katika kaunti ya Makueni. Taarifa kutoka maeneo yote 70 zitachambuliwa na kuwekwa katika ripoti kila mwezi, ambayo itasambazwa kwa watu wengi (lakini jina na namba ya simu ya washiriki vitatunzwa kisiri). Ripoti hiyo pia itapelekwa kwenye vyombo vya habari. Kwa njia hii, wananchi wengi, viongozi, wawakilishi, na hata Rais watafahamu ukweli juu ya kile kinachotokea katika jamii na watasikia mawazo ya wananchi.

Wakati fulani viongozi hufanya maamuzi bila kujua ukweli wa hali ya maisha ya watu. Sauti za Wananchi ni jitihada itakayohakikisha kwamba ukweli na sauti vinasikika.

# Wahusika:



Timothy

Mjasiriamali, muongozaji wa eneo la zoezi.



Musyoka

Mmoja wa washiriki.




Nthenya

Mratibu wa kikundi cha washiriki wa zoezi la Sauti za Wananchi.



Muthoka

Mwananchi mwenye mashaka na utafiti.



Watafiti

Waratibu wa awali wa Sauti za Wananchi.


Huyu Musyoka hajaja kuchukua baiskeli yake...
Ah, kwani hujui? Kapata wageni.
Fundi BASKELI SAFI HAPA
Wametoka wapi?


Sijui, alipokea vijana wakiwa na mabegi na maboksi.
Dili gani hilo? Twendeni tukacheki!
Dili!


Nyumbani kwa Musyoka.
Mzee, umechaguliwa kushiriki katika zoezi la Sauti za Wananchi.
Nashukuru... Lakini linahusu nini wanangu?
B


Sauti za Wananchi inalenga kufahamu ukweli kutoka kwa wananchi.
Lakini mimi siyo mtaalam...
Wala haihitaji utaalam. Zoezi hili linalenga kuwasikiliza wananchi.


Mmh, nitaulizwa nini?
Maswali ya kawaida kuhusu hali halisi ilivyo, na kupata maoni yako.



Nani anasimamia utafiti huo?
Utafiti unasimamiwa na shirika huru la Twaweza.
Matokeo kwa ujumla yatawekwa hadharani, lakini majina ya wanaohojiwa yote yatabaki siri.
Ahaa!


Wakikaribia mwisho...
Musyoka, tutawasiliana nawe kwa kutumia simu hii kati ya mara moja mpaka nne kwa mwezi.
Oooh! Asante sa...
Hodi! Hodi! Musyoka!


Bwana Fundi, umenijia na kikosi kabisa... Karibuni!
Ndiyo Mzee, nasi tumefuata zawadi za wageni!
Acha utani kaka. Tuko hapa katika shughuli ya utafiti.


Mbona sisi hatumo, au mnabagua?
Tuliandaa orodha ya nyumba zote katika eneo hili, kisha tukachagua kaya 12 tu kwa njia ya kinasibu.


Sasa kwa nini mnawapa hizo simu?
Zoezi hili lina awamu mbili. Mahojiano haya ni ya awali. Baadaye tutakusanya taarifa mara kwa mara kwa njia ya simu.


Hakuna umeme hapa kijijini, ataichaji wapi simu?
Kila kikundi cha washiriki kitapewa vifaa vya kuchaji simu kwa umeme wa jua.
Ahaa, kumbe!
Safi sana!

## Kikao cha washiriki wote...




Swali zuri! Huyo atatusaidia pale wewe au jirani yako hapatikani kwenye simu au kama kapata dharura.
Enhe, naona kuna mkono...


Tusisahau kuwa kiongozi atachaguliwa kutoka kwa washiriki hawa kumi na wawili.
Basi tumchague **Nthenya** Au sio jamani?
Anafaa! Huyohuyoo! Kabisaa!


Tutapata nini kwa kushiriki?
Hii ni fursa ya kipekee kutoa sauti ili umma uelewe hali halisi.
Inawezekana kweli?


Sijaelewa, ki vipi?
Zoezi la Sauti za Wananchi linahusisha watu 840 katika kauti ya Makueni. Maoni hayo yataunganishwa na kutolewa hadharani kupitia vyombo vya habari.


Oh, tulisahau kuuliza. Majina yetu yatatangazwa hadharani?
Hapana, majina yenu ni siri kati yenu na sisi tu.


Ni hilo tu?
Utakaposhiriki kikamilifu, utaongezewa muda wa maongezi kwenye simu yako.
Na ukishiriki kikamilifu, mwisho wa utafiti huu simu itakuwa mali yako!


Kuna motisha gani kwa kikundi?
Wanakikundi wote wakishiriki kwa mara 3 mfululizo, washiriki wote watazawadiwa muda wa maongezi zaidi.


Zoezi hili litadumu kwa siku ngapi?
Si siku, ni takriban miaka miwili!


Kwa watakaoshiriki kila mara bila kukosa, washiriki angalau 100 watachaguliwa na kuzawadiwa redio za kisasa. Haya kazi kwenu!
Hii kitu sitoiacha inipite!


Tukiwa na maswali zaidi tuwasiliane na nani?
Mnaweza kupiga simu au kutuma ujumbe kwenda namba 0725933249 au 0722369856


Haya jamani, kila la heri...
Tunashukuru sana!


Nimepata bahati adimu sana. Kati ya wananchi wote katika kaunti ya Makueni, maoni yangu yatasikika!
Hiyo ni kweli kabisa!
B

## Fuata hatua hizi ili kuboresha mawasiliano:



- Pokea simu yako ukipigiwa
- Chagua mahali kwenye utulivu upokeapo simu
- Chagua muda mwafaka wa kufanya mahojiano
- Ondoa au kaa mbali na usumbufu
- Kamata simu yako kwa namna ambayo utaweza kusikika na wewe kusikia
- Msikilize kwa makini mtu unayewasiliana nae
- Iwapo haujasikia vizuri muulize anayeongea na wewe arudie
- Uliza maswali iwapo hujaelewa
- Ongea kwa sauti ya wastani.



## Jinsi ya kuhakikisha simu inakuwa na chaji muda wa kutosha:

- Usizime na kuwasha simu kila mara
- Usiiweke simu yako kwenye hali ya kutingishika ikipigwa
- Punguza mwanga wa kioo (skrini) cha simu yako
- Unaposikiliza redio tumia spika za masikioni (ear phone) badala ya spika ya kwenye simu
- Tumia mwanga wa tochi mara chache.